# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## WAKALA WA SERIKALI MTANDAO (eGAZ)

# "Zanzibar Government Electronic Payment Gateway"

# (ZanMalipo)

## TARATIBU NA MGAWANYO WA MAJUKUMU YA MFUMO MKUU WA SERIKALI WA UKUSANYAJI MAPATO KIELEKTRONIKI

**TOLEO LA KWANZA (Ver. 1.0.1)**

**Imeandaliwana : Zanzibar e-Government Agency**

# Table of Contents

Table of Contents ........ 2

1.0 Utangulizi` ........ 3

2.0 Watumiaji wa Mfumo ........ 3

3.0 Namna ya kujiunga na Mfumo ........ 3

3.1 Kwa Taasisi zenye Mfumo wa Kuandaa Madai (Billing System) ........ 3

3.1 Kwa Taasisi zisizo na Mfumo wa Kuandaa Madai (Billing System) ........ 5

4.0 Mgawanyo wa Majukumu ........ 6

4.1 Wakala wa Serikali Mtandao(eGAZ)-Zanzibar ........ 6

4.2 Wizara, Idara Wakala na Taasisi za Serikali ........ 6

## 1.0 Utangulizi`

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Kupitia Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ), wametengeneza Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato uitwao kwa jina la **Zanzibar *Government Electronic Payment Gateway*** unaojulikana kama ZanMalipo.

Mfumo huu umekamilika na tayari baadhi ya taasisi za Serikali zimeshaanza kukusanya mapato kupitia Mfumo wa ZanMalipo. Aidha, watoa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na mabenki na mitandao ya simu wameshirikishwa ili kufanikisha utekelezaji wa azma ya Serikali.

## 2.0 WATUMIAJI WA MFUMO

Mfumo huu utatumiwa na wananchi wa kawaida (walipaji wa huduma mbalimbali za Serikali), Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Manispaa pamoja na Halmashauri zote Miji za Zanzibar. Aidha mfumo utaweza kutoa ripoti mbalimbali za makusanyo ya Mapato kwa umma.

## 3.0 NAMNA YA KUJIUNGA NA MFUMO

### 3.1. KWA TAASISI ZENYE MFUMO WA KUANDAA MADAI (BILLING SYSTEM)

3.1.1. Jaza fomu ya kuomba kujiunga kwenye Mfumo wa ZanMalipo inayopatikana katika tovuti ya www.zanmalipo.go.tz pia kupitia tovuti ya Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) www.egoz.go.tz.

3.1.2 Unganisha Mfumo wa Taasisi yako na mfumo wa ZanMalipo kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) - Zanzibar.

3.1.3 Kuwasilisha matokeo ya majaribio ya kuunganisha Mfumo wa Taasisi na ZanMalipo (Test Cases Results) ili Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ)- Zanzibar ili yatumike katika kufanya maamuzi ya kuunganisha Taasisi na ZanMalipo kwenye mazingira halisi ya kazi.

3.1.4 Andaa Mafunzo ya Mfumo unaotumiwa na Taasisi yako katika kuandaa Bili pamoja na Mafunzo ya jinsi ya kutumia ZanMalipo kwa watumiaji wako wote, ambayo yatagharimiwa na taasisi yako. Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) Zanzibar itatoa wawezeshaji wasiozidi wawili (2) kwa ajili ya kuendesha mafunzo ya ZanMalipo.

3.1.5 Wasilisha taarifa za akaunti za mapato (Mfano: Jina la akaunti, Jina la Benki, Namba ya akaunti na aina ya akaunti). Unashauriwa usiwe na akaunti zaidi ya moja (1) kwa benki moja kwa Sarafu moja (1). Pia wasilisha taarifa za akaunti ya Makusanyo ya Taasisi yako iliyoko Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

3.1.6 Unashauriwa kufungua akaunti za makusanyo kwenye Benki zaidi ya moja na kuziwasilisha, ili kuwarahisisishia walipaji wa huduma za Serikali na pia kuepuka usimamishaji wa makusanyo ya Serikali pale benki moja inapokuwa na tatizo. Akaunti zitakazowasilishwa ziwe kwenye benki ambayo tayari imeunganishwa na Mfumo wa ZanMalipo.

3.1.7 Andaa orodha na bajeti ya vyanzo vya Mapato (Revenue Sources and Targets) kabla ya kuwasilisha vyanzo vya mapato kwa Wakala wa Serikali Mtandao hakikisha orodha umeiwasilisha , (OR) Fedha na Mipango , Idara ya Bajeti kwa uhakiki .

3.1.8 Andaa orodha ya vituo vya makusanyo ya mapato (Revenue Collection Centers)

3.1.9 Wasilisha majina ya maafisa TEHAMA wawili (2) ambao watasimamia Mfumo huu katika Taasisi yako kwa kujaza fomu ya kusajili ya watumiaji (User Registration Form) inayopatikana kwenye tovuti ya ZanMalipo.

3.1.10 Andaa ratiba utakayoitumia kufanya majaribio ya kuunganisha Mfumo wako na ZanMalipo. Ratiba hiyo iainishe idadi ya siku, tarehe na muda ambapo majaribio hayo yatafanyika.

## 3.2. KWA TAASISI ZISIZO NA MFUMO WA KUANDAA MADAI (BILLING SYSTEM)

3.2.1. Jaza fomu ya kuomba kujiunga kwenye Mfumo wa ZanMalipo inayopatikana kwenye tovuti ya ZanMalipo na pia kupitia tovuti ya Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ)-Zanzibar. Andaa bajeti ya Mafunzo ya Mfumo wa ZanMalipo ambayo yatagharimiwa na **taasisi yako.**

3.2.2. Wasilisha taarifa za akaunti za mapato (Mfano: Jina la akaunti, Jina la Benki, Namba ya akaunti na aina ya akaunti). Unashauriwa usiwe na akaunti zaidi ya moja (1) kwa benki moja kwa Sarafu moja (1). Pia wasilisha taarifa za akaunti ya Makusanyo ya Taasisi yako iliyoko Benki Kuu ya Tanzania.

3.2.3. Unashauriwa kufungua akaunti za makusanyo kwenye Benki Zaidi ya moja na kuziwasilisha, ili kuwarahisishia walipaji wa huduma za Serikali na pia kuepuka usimamishaji wa makusanyo ya Serikali pale benki moja inapokuwa na tatizo. Akaunti zitakazowasilishwa ziwe kwenye benki ambayo tayari imeunganishwa na Mfumo wa ZanMalipo.

3.2.4. Andaa orodha na bajeti ya vyanzo vya Mapato (Revenue Sources and Targets) kabla ya kuwasilisha vyanzo vya mapato kwa Wakala wa Serikali Mtandao hakikisha orodha umewasilisha (OR) Fedha na Mipango, Idara ya Bajeti kwa uhakiki

3.2.5. Andaa orodha ya vituo vya makusanyo ya mapato (Revenue Collection Centers)

3.2.6. Wasilisha majina ya maafisa TEHAMA wawili (2) ambao watasimamia Mfumo huu katika Taasisi yako kwa kujaza fomu ya kusajili ya watumiaji (User Registration Form) inayopatikana kwenye tovuti ya ZanMalipo.

## 4.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU

### 4.1. WAKALA WA SERIKALI MTANDAO (EGAZ)-ZANZIBAR

4.1.1 Usimamizi wa Mfumo kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa Mfumo unapatikana wakati wote na watumiaji wanapatiwa msaada wakiufundi kila unapohitajika.

4.1.2 Usimamizi wa usalama wa Mfumo ikiwa ni pamoja na miamala yote inayofanyika kupitia mfumo huu.

4.1.3 Kutoa viwango vya kuunganisha Mfumo wa ZanMalipo na Mifumo mingine inayohitaji kuunganishwa (ZanMalipo Integration Standards including APIs, Integration Test Cases).

4.1.4 Kutoa elimu ya matumizi bora ya mfumo kwa watumiaji wote.

4.1.5 Kuufanyia maboresho mfumo pale yanapohitajika.

### 4.2 WIZARA, IDARA WAKALA NA TAASISI ZA SERIKALI

4.2.1 Wasilisha kwa Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ)-Zanzibar, taarifa zote muhimu zinazohitajika ili kuisajili Taasisi na kuanza kutumia mfumo

4.2.2 Kusimamia majukumu yote ya ukusanyaji wa mapato ya Taasisi husika

4.2.3 Kusimamia akaunti zote za ukusanyaji Mapato

4.2.4 Kufanya usuluhishi wa taarifa za miamala ya makusanyo (Revenue Transaction Reconciliation)

4.2.5 Kusimamia watumiaji wa mfumo katika taasisi husika ikiwa ni pamoja na kuwasajili/ kuwaondoa na kuwapangia majukumu ndani ya mfumo.

4.2.6 Kutoa taarifa mapema kwa Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) Zanzibar, juu ya changamoto zozote zinazohusu mfumo kwa kutumia namba **255 24 22 35688** kwabarua pepe **info@zanmalipo.go.tz**.

4.2.7 Kutoa taarifa iwapo fedha hazijahama kwa wakati kutoka akaunti ya makusanyo ya benki ya biashara kwenda Benki kuu ya Tanzania.